JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA


OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MUHTASARI WA KIKAO CHA KWANZA CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA

TAREHE 25 NOVEMBA, 2020.











Imetayarishwa Na:

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,

S.L.P. 1054,
LINDI.
Barua pepe: ras.lindi@tamisemi.go.tz
Simu Na. 023 220 2502
023 220 2098
Fax Na. 023 220 2502

Machi, 2022

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KWANZA CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA KILICHOFANYIKA UKUMBI WA OFISI YA MKUU WA MKOA TAREHE 25.11.2020.**

**A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mhe. Godfrey W. Zambi | Mkuu wa Mkoa | Lindi | M/Kiti |
| 2 | Bi. Rehema S. Madenge | Katibu Tawala Mkoa | Lindi | Katibu |
| 3 | Mhe. Sarah V. Chiwamba | Mkuu wa Wilaya | Liwale | Mjumbe |
| 4 | Mhe. Hashimu Mgandilwa | Mkuu wa Wilaya | Ruangwa | Mjumbe |
| 5 | Mhe. Shaibu Ndemanga | Mkuu wa Wilaya | Lindi | Mjumbe |
| 6 | Mhe. Hashim A. Komba | Mkuu wa Wilaya | Nachingwea | Mjumbe |
| 7 | Mhe. Christopher E. Ngubiagai | Mkuu wa Wilaya | Kilwa | Mjumbe |
| 8 | Mhe. Salma R. Kikwete | Mbunge | Mchinga | Mjumbe |
| 9 | Mhe. Zuberi Kuchauka | Mbunge | Liwale | Mjumbe |
| 10 | Mhe. Dkt. Amadaus J. Chinguile | Mbunge | Nachingwea | Mjumbe |
| 11 | Mhe. Nape M. Nnauye | Mbunge | Mtama | Mjumbe |
| 12 | Mhe. Ally M. Kassinge | Mbunge | Kilwa Kus. | Mjumbe |
| 13 | Mhe. Hamida M. Abdallah | Mbunge | Lindi (M) | Mjumbe |
| 14 | Mhe. Francis K. Ndulane | Mbunge | Kilwa Kask. | Mjumbe |
| 15 | Mhe. Francis Magali (Frank) | Mstahiki Meya | Manispaa ya Lindi | Mjumbe |
| 16 | Ndg. Luiza O. Mlelwa | Mkurugenzi Mtendaji | Liwale | Mjumbe |
| 17 | Ndg. Frank F. Chonya | Mkurugenzi Mtendaji | Ruangwa | Mjumbe |
| 18 | Ndg. Renatus B. Mchau | Mkurugenzi Mtendaji | Kilwa | Mjumbe |
| 19 | Ndg. Hassan A. Rugwa | Mkurugenzi Mtendaji | Nachingwea | Mjumbe |
| 20 | Ndg. Jomaary M. Satura | Mkurugenzi wa Manispaa | Lindi | Mjumbe |
| 21 | Ndg. Mahamud A. Kimbokota | K/Mkurugenzi Mtendaji | Mtama | Mjumbe |

**B: WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Mhe. Kassim M. Majaliwa | Mbunge | Ruangwa |

C: **WAALIKWA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Ndg. Abasi A. Matulilo | Mwenyekiti CCM (M) | Liwale |
| 2 | Ndg. Innocent M. Nanzabar | Katibu CCM (M) | Lindi |
| 3 | ACP Mtatiro Kitinkwi | Kamanda wa Polisi – Mkoa | Lindi |
| 4 | ACP DR. Sylvester Shija | Kamanda wa Magereza (M) | Lindi |
| 5 | Maj. Ramadhani A. Makowa | Mshauri Jeshi la Akiba (M) | Lindi |
| 6 | Ndg. Elirehema Nyiti | Afisa Usalama (M) | Lindi |
| 7 | Ndg. Charles Mulebya | Kaimu Kamanda wa TAKUKURU Mkoa | Lindi |
| 8 | ACI. Cleth M. Mumwi | Kamanda wa Uhamiaji (M) | Lindi |
| 9 | Insp. Joseph J. Ngonyani | K/Mkuu wa Zimamoto na Uokoaji (M) | Lindi |
| 10 | Ndg. Hassani H. Shomari | Msaidizi wa Magereza (M) | Lindi |
| 11 | Ndg. Feisal A. Juma | Msaidizi wa Kamanda wa Polisi (M) | Lindi |
| 12 | Ndg. Dedan Jonas | Mfamasia (M) | Lindi |
| 13 | Ndg. Zainab Mathradas | Mratibu wa Afya ya mama na mtoto Mkoa | Lindi |
| 14 | Ndg. Neema Magambo | Mkuu wa Tawi la Chuo Kikuu Huria | Lindi |
| 15 | Ndg. Beatha Kessy | Mratibu Msaidizi wa huduma za Mama na Mtoto – Mkoa | Lindi |
| 16 | Ndg. Salum Halfani | Kaimu Meneja (M) – CRDB | Lindi |
| 17 | Ndg. Kibabu Seiph | Afisa Habari UVCCM – (M) | Lindi |
| 18 | Ndg. Kulwa James | Kaimu Afisa Elimu (M) | Lindi |
| 19 | Ndg. Mariam Kaisi | Mwenyekiti TCCIA | Lindi |
| 20 | Ndg. Juma J. Hamadi | Kaimu Afisa Mipango | Kilwa |
| 21 | Ndg. Jeremiah Hango | Afisa Madini Mkoa | Nachingwea |
| 22 | Ndg. Nurdin Mchinjo | Mhasibu | Lindi RS |
| 23 | Ndg. Fred Kahisha | Afisa Manunuzi | Lindi RS |
| 24 | Ndg. Stephen A. Masawe | Meneja Vipimo - Mkoa | Lindi |
| 25 | Ndg. Richard A. Shabani | Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa | Lindi |
| 26 | Ndg. Idrisa I. Kafunzi | Mhakikimali (M) | Lindi |
| 27 | Ndg. Salama Z. Kitumbo | Mwakilishi wa TARUCHINA | Lindi |
| 28 | Ndg. Denis Venance | Kaimu Mkuu wa kitengo cha TEHAMA | Lindi RS |
| 29 | Ndg. Neema Konzo | Afisa Utumishi | Lindi RS |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 30 | Eng. Emmanuel Sengwaji | Kaimu Meneja – TANESCO | Lindi |
| 31 | Ndg. Nassoro Mwinshehe | Katibu CWT (M) | Lindi |
| 32 | Ndg. Bongi Ahmed | Mhasibu (M) | Lindi RS |
| 33 | Ndg. Prisca Unga | Mkurugenzi LISAWE | Lindi |
| 34 | Ndg. Prosper M. Roman | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Serikali za Mitaa | Lindi RS |
| 35 | Ndg. Victor M. Mimbi | Afisa Biashara | Lindi RS |
| 36 | Ndg. Julius Ndele | Mchumi | Lindi MC |
| 37 | Ndg. Juma Mleli | Afisa Mfawidhi tume ya haki za Binadamu | |
| 38 | Ndg. Thomas Safari | Katibu Tawala Wilaya | Lindi |
| 39 | Ndg. Emmanuel Mwikwabe | Meneja (M) NHIF | Lindi |
| 40 | Ndg. Humphrey Kiwia | Meneja (M) TTCL | Lindi |
| 41 | Ndg. Beatrice Nagunwa | Kaimu Meneja wa Tawi –NIC | Lindi |
| 42 | Ndg. Christina Shayo | Meneja (M) TBA | Lindi |
| 42 | Ndg. Neema E. Ngonyani | Mwakilishi wa Hakimu Mfawidhi | Lindi |
| 44 | Ndg. Rashid Kikupwa | Katibu UPDP (M) | Kilwa |
| 45 | Ndg. Erick P. Nyagali | Afisa wa Bandari | Lindi |
| 46 | Ndg. Said Kijiji | Kamishina Msaidizi wa Ardhi (M) | Lindi |
| 47 | Ndg. Bakari M. Mlona | Katibu CHAWATA (M) | Lindi |
| 48 | Ndg. Mohamed C. Ngemage | Mwakilishi wa AMCOS | Ruangwa |
| 49 | Ndg. Kheri Joshua | Kaimu Meneja Vipimo | Mtwara |
| 50 | Eng. Tengamaso Wilson | Mhandisi | Lindi RS |
| 51 | Ndg. Bora Mchilassi | Kaimu Meneja NMB | Lindi |
| 52 | Dkt. Bora Gretha Haule | Katibu Tawala Msaidizi Utawala na Rasilimali watu | Lindi RS |
| 53 | Eng. Lubasa S.M | Meneja RUWASA (M) | Lindi |
| 54 | Eng. Dawson K. Paschal | Kaimu Mratibu wa Mkoa TARURA | Lindi |
| 55 | Ndg. Richard Uswege | Afisa Uvuvi | Lindi RS |
| 56 | Ndg. Jafari Meraji | Meneja (M) PSSSF | Lindi RS |
| 57 | Ndg. Daud Jackson | Afisa Tehama | Lindi RS |
| 58 | Ndg. Fundikira L. Masamalo | Afisa Mipango | Ruangwa |
| 59 | Eng. Jumbe J. Kiboni | RIO | Lindi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 60 | Ndg. Makalage S. Nkinda | Afisa Utamaduni | Lindi RS |
| 61 | Ndg. Salima R. Ally | SIDO | Lindi |
| 62 | Ndg. Pili Kamali | Mkuu wa Hazina Ndogo | Lindi |
| 63 | Ndg. Musa Mziya | Meneja BOT | Mtwara |
| 64 | Ndg. Sarah F. Kasongwa | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Lindi RS |
| 65 | Ndg. Gibson Mwaigomole | Meneja (M) NHC | Lindi |
| 66 | Ndg. Ally Angelo | Mwakilishi NBC | Lindi |
| 67 | Ndg. Ayubu A. Pero | Katibu Tawala Wilaya | Ruangwa |
| 68 | Ndg. Omary S. Mwanga | Katibu Tawala Wilaya | Nachingwea |
| 69 | Ndg. Mustapha H. Nchia | Mwenyekiti SHIVYAWATA | Lindi |
| 70 | Dkt. Alfred Magani | Mkuu wa chuo COTC | Lindi |
| 71 | Ndg. Jonaphrey Pembe | Mwenyekiti LIWOPAC | Lindi |
| 72 | Ndg. Nicodemus Mwakilembe | Meneja (M) TRA | Lindi |
| 73 | Ndg. Kassongo Kutapa | Afisa huduma na elimu kwa walipakodi –TRA | Lindi |
| 74 | Ndg. Rashidi Kikupwa | Mwenyekiti UPDP (M) | Lindi |
| 75 | Ndg. Nnunduma Abdallah | Afisa Mipango | Nachingwea |
| 76 | Ndg. Omari B. Chinguile | Afisa Mipango | Liwale |
| 77 | Ndg. Halifa A. Magao | Mwakilishi toka LCIO | Liwale |
| 78 | Ndg. Rashidi Mohamedi | Mkulima | Mtama |
| 79 | Ndg. Shaibu N. Mnyanga | Mwenyekiti NCCR | Chikonji |
| 80 | Ndg. Idrisa H. Senulo | Kaimu meneja LUWASA | Mtama |
| 81 | Ndg. Cleophas Sikada | Kaimu mkuu wa chuo VETA | Lindi |
| 82 | Ndg. Fortunatus A. Mruice | Kaimu Meneja (M) TEMESA | Lindi |
| 83 | Ndg. Frumence Mushi | Meneja (M) TPB Bank | Lindi |
| 84 | Ndg. Ahmad M. Rashid | Meneja (M) TPC | Lindi |
| 85 | Ndg. Juma Yusuph | Ag. APM CBT | Lindi |
| 86 | Ndg. Ephatar Mlavi | Meneja (M) TANROADS | Lindi |
| 87 | Ndg. Robert E. Mosea | Engineer TANROADS | Lindi |
| 88 | Ndg. Juma R. Judifa | Mwenyekiti Soko Kuu | Lindi |
| 89 | Ndg. Bakari H. Swalehe | Afisa Tawala | Lindi RS |
| 90 | Ndg. Ridhiwani Yusuf | Mtunza Kumbukumbu | Lindi RS |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 91 | Ndg. Grace Mahundu | Katibu Muhtasi | Lindi RS |
| 92 | Ndg. Edwin A. Ngongolowo | Mhasibu | Lindi RS |

**D. SEKRETARIETI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Ndg. Scola A. Mwalyanzi | K/K/Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu | Lindi RS |
| 2 | Ndg. Gaudence Nyamwihura | A/Maendeleo ya Jamii Mkuu | Lindi RS |
| 3 | Ndg. Saidi H. Chotimbao | Mchumi | Lindi RS |
| 4 | Ndg. Maria Kasiga | Mtakwimu | Lindi RS |
| 5 | Ndg. Jumbe Kawambwa | Afisa Uvuvi | Lindi RS |
| 7 | Ndg. Athuman Mbwago | Mhudumu | Lindi RS |

**Muht. Na. 01/11/2020: Kufungua Kikao**

Kabla ya kufungua kikao, mwenyekiti alianza kwa kutoa shukrani kwa wajumbe na waalikwa kwa mahudhurio mazuri na kufika kwa wakati.Aidha, aliwakumbusha wajumbe kuwa kikao cha mwisho kilifanyika tarehe 28 Februari, 2020 na kikao kingine kilitakiwa kufanyika baada ya miezi sita. Hata hivyo hakikuweza kufanyika kutokana na wajumbe wengi ambao ni Wabunge, Meya na Wenyeviti wa halmashauri kutokuwepo wakati wa mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Alitoa pongezi kwa waheshimiwa wabunge ambao walihudhuria kwa mara ya kwanza baada ya kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 na wao kuchaguliwa kwa kishindo. Aliwakumbusha wajumbe kuwa kikao cha RCC ni kikao kikubwa katika mkoa na kinajadili masuala yote ya maendeleo ya mkoa katika sekta zote na ndiyo maana wakuu wa taasisi za umma na wakuu wa idara za Sekretarieti ya mkoa wanatakiwa kushiriki. Aidha, aliwataka wawakilishi wa TANESCO kujiandaa kutoa majibu kwa wajumbe juu ya sababu za kukatika katika kwa umeme katika mkoa wa Lindi kwani bado kuna malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali na hii haileti taswira nzuri katika jamii ya wana Lindi.

Aliwataarifu wajumbe kuwa kwenye suala la elimu tayari matokeo ya mtihani wa darasa la saba yalikuwa yametoka na mkoa wetu umekuwa mmoja kati ya mikoa mitatu nchini iliyoongeza ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo. Alieleza kuwa mwaka huu mkoa wetu umeingiza halmashauri moja katika halmashauri zinazofanya vizuri nchini ambapo

halmashauri ya Nachingwea imeingia kwenye nafasi hiyo. Alitoa taarifa kuwa mitihani ya kidato cha nne tayari imeanza na viongozi wamekuwa wakiendelea kuwatia moyo wanafunzi wanaojiandaa kufanya mitihani ili wafanye vizuri

Baada ya kueleza hayo aliwataka wajumbe na waalikwa ambao ni mara yao ya kwanza kushiriki kusimama na akamtambulisha kamanda wa polisi wa mkoa ACP Mtatiro Kitinkwi aliyehamia kutoka mkoa wa Geita

Mwenyekiti alieleza masikitiko yake kutokana na kitendo cha afisa wa LATRA Ndugu Manase cha kumshikia panga dereva wa gari akimtuhumu kwa makosa ya usalama barabarani. Kimsingi alisema kuwa alipata tuhuma za mienendo ya mtumishi huyo hata kabla ya tukio hilo, alimuita na kumuonya mara kadhaa kumkumbusha kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu lakini hakutaka kubadilika

Alitumia fursa hiyo kuwakumbusha maafisa wa serikali kuwa hakuna aliye juu ya sheria na kila mmoja anapaswa kuwatumikia wananchi kwa unyenyekevu kwa kufuata sheria kanuni, taratibu na miongozo iliyowekwa na kuwataka wakuu wa wilaya kusimamia sheria kwenye maeneo yao. Mwisho alifungua rasmi kikao mnamo saa 3 13 asubuhi

**Muht. Na. 02/11/2020: Kuridhia agenda za kikao cha kwanza 2020/2021**

Mwenyekiti aliwapitisha wajumbe kwenye ajenda zilizoandaliwa na wajumbe waliridhia ajenda zilizoandaliwa

**Muht. Na. 03/11/2020: Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 28 Februari, 2020**

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia muhtasari huo ukurasa kwa ukurasa. Marekebisho yafuatayo yalifanyika,-

Ukurasa wa 3 jina nambari 8 linalosomeka ***Mh. Salma Kikwete*** lisomeke Mh. Salma Rashid Kikwete, katika ukurasa wa 8 panaposomeka "….***wajumbe waliokuwa wamejiandikisha katika kitabu cha mahudhurio walikuwa 22 dhidi ya wajumbe 34 wa kikao…***" isomeke wajumbe waliokuwa wamejiandikisha katika kitabu cha mahudhurio walikuwa 28 dhidi ya wajumbe 33 wa kikao. Katika ukurasa wa 17 panaposomeka "***Mapato ya ndani yanayokwenda kwenye utekelezaji wa miradi ya wanawake na vijana 10%***",

pasomeke Mapato ya ndani yanayokwenda kwenye utekelezaji wa miradi ya wanawake na vijana na watu wenye ulemavu 10%. Baada ya masahihisho hayo, muhtasari ulithibitishwa kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao hicho.

**Muht. Na. 04/11/2020:Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya kikao cha tarehe 28 Februari, 2020**

Katika kujadili yatokanayo na kikao cha tarehe 28/02/2020 yafuatayo yalijitokeza:-

**Utekelezaji wa mipango ya ukarabati wa majosho:**

Wajumbe walishauri kuwa suala hili liwe endelevu na liendelee kuripotiwa kwa kuonesha asilimia ya utekelezaji kwenye kila kikao badala ya kuripoti mipango iliyowekwa kwenye halmashauri. Aidha, halmashauri ya Mtama iangalie uwezekano wa kuwa na josho kwani kwa sasa idadi ya mifugo inaongezeka kwa kasi kubwa katika halmashauri hiyo.

**Ujenzi wa vituo vya mabasi:**

Wakurugenzi wa Kilwa na Nachingwea wahakikishe ujenzi wa vituo vya mabasi vya halmashauri Kilwa (Nangurukuru) na Nachingwea unakamilika katika kipindi cha miezi mitatu. Pia Mkurugenzi wa halmashauri ya Mtama alishauriwa asimamie ujenzi wa kituo cha mabasi kwa kutumia Tsh. Milioni 200 zilizotengwa katika bajeti na kazi hii ikamilike katika kipindi cha miezi mitatu.

**Umiliki wa Ardhi:**

Wajumbe walijadili kwa kina suala la miliki ya ardhi kwa taasisi za umma na kushauri kuwa wakuu wa taasisi zote za umma wahakikishe kuwa ndani ya miezi 6 maeneo yote wanayomiliki yawe yamepimwa kwenye halmashauri zote na kupatiwa hati miliki. Aidha, kwa wale ambao hawataendeleza maeneo waliyopatiwa, sheria ya ardhi na maendelezo ya viwanja itumike.

**Kituo ch afya Kipatimu:**

Wajumbe walipokea utekelezaji wa agizo la kushughulikia malalamiko ya wananchi kuhusiana na huduma zinazotolewa na kituo cha Afya Kipatimu. Kwa pamoja walikubaliana kuwa ipo haja ya kukutana na Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki Lindi ili kujadiliana kwa kina juu ya huduma zinazotolewa katika kituo hicho

Kwa upande wa mipaka ya halmashauri ya manispaa kubadilika baada ya eneo la jimbo la Mchinga kuingizwa katika mipaka ya kijiografia ya Manispaa kutokea Mtama ilionekana ipo haja ya kutoa tafsiri katika ngazi mbali mbali hususan mipaka ya kiutawala. Aidha, ilifafanuliwa kuwa kwa upande wa Chama Cha Mapinduzi tayari kamati za siasa za mkoa, na wilaya zote mbili zilipanga kukutana kwa pamoja ili kuwa na uelewa wa pamoja baada ya mgawanyo huo wa mipaka.

**Maagizo/Maazimio**

i. **Mkurugenzi wa halmashauri ya Mtama ahakikishe kuwa Tsh. Milioni 200 zilizotengwa katika bajeti zinaelekezwa katika ujenzi wa kituo cha mabasi na kazi iwe imekamilika katika kipindi cha miezi mitatu toka tarehe ya kikao.**

ii. **Katika kipindi cha miezi mitatu Wakurugenzi wa halmashauri za Kilwa na Nachingwea wakamilishe ujenzi wa vituo vya mabasi vya Nangurukuru – Kilwa na Nachingwea.**

iii. **Halmashauari ya Wilaya ya Kilwa iweke katika mipango yake ujenzi wa kituo cha Afya Kipatimu.**

**Muht. Na. 05/11/2020: Taarifa ya uchaguzi Mkuu Oktoba, 2020**

Taarifa ilionyesha kuwa katika uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba 2020, katika mkoa wa Lindi kulikuwa na majimbo ya uchaguzi 8 (Lindi Mjini, Mchinga, Kilwa Kaskazini, Kilwa Kusini, Liwale, Nachingwea, Ruangwa na Mtama) na kata 152. Mkoa ulikuwa na jumla ya vituo 1,924 vyenye wapiga kura 646,922.

Taarifa ilionesha kuwa Mgombea wa Urais kupitia CCM Dkt John Pombe Joseph Magufuli alipata kura 285,307 kati ya kura halali 381,198 sawa na asilimia 75 na kwa upande wa ubunge wagombea wa CCM walishinda katika majimbo yote 6 yaliyofanya uchaguzi na majimbo mawili walipita bila kupingwa. Kuhusu nafasi za udiwani katika kata 140 zilizofanya uchaguzi CCM ilishinda kata 125, kata 12 walipita bila kupingwa, ACT – Wazalendo kata 5, CHADEMA kata 7, na CUF kata 2.

Taarifa ilipokelewa na wajumbe waliijadili kwa kirefu na wengi waliochangia walieleza masikitiko yao juu ya fujo zilizotokea Liwale, Mtama na Nachingwea. Pamoja na mali za raia kuharibiwa ilielezwa kuwa magari ya serikali na ofisi viliharibiwa kwa kuchomwa moto na athari iliyopo ni kubwa na haiwezi kufumbiwa macho.

kwani matukio kama haya yamekuwa yakijirudia mara kwa mara katika maeneo ya mkoa wa Lindi. Kufuatia hasara ya upotevu wa mali ushauri ulitolewa juu ya kutoa elimu ya bima kwa wananchi ili kuepuka hasara kwa nyakati zijazo.

**Maagizo/Maazimio**

i. **Kamanda wa polisi wa mkoa afuatilie mienendo ya majalada yote ya uchunguzi na kuhakikisha kuwa wote waliohusika wanakamatwa, uchunguzi kukamilika na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria ili haki itendeke.**

ii. **Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Lindi kupitia Kamati ya Usalama ya wilaya ya Lindi ahakikishe kuwa anafuatilia suala la mtuhumiwa aliyekamatwa na kuachiwa na ikishindikana suala hilo lipelekwe kwenye Kamati ya Usalama ya Mkoa.**

**Muht. Na. 06/11/2020: Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kuanzia mwaka 2019/2020 hadi Oktoba, 2020**

Taarifa ilionesha kuwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 mkoa uliidhinishiwa kutumia Jumla ya Tsh.**130,983,945,011.04/=**, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 kiasi cha Tsh.**122,916,718,089.00/=** kilikuwa kimepokelewa ambacho ni sawa na asilimia 93 ya kiasi kilichopokelewa na mkoa.

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2020/2021 KUANZIA JULAI, 2020 HADI OKTOBA, 2020.**

Taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2020/2021 kuanzia Julai, 2020 hadi Oktoba, 2020 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ilionesha kuwa mkoa uliidhinishiwa kutumia Jumla ya Tsh. **162,026,703,500.00/=**. Hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2020 kiasi cha Tsh.**40,687,080,858.00 /=** sawa na asilimia 25 kilikuwa kimetolewa.

**Muht. Na. 07/11/2020: Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kuanzia Julai, 2020/2021 hadi Oktoba, 2020**

Taarifa ya utekelezaji ilitolewa kwa kila sekta kama ifuatavyo -

**SEKTA YA KILIMO**

Katika sekta ya kilimo kwa mwaka 2019/20 mkoa ulifanikiwa kupata jumla ya tani 543,514 za uzalishaji katika mazao ya chakula na biashara sawa na asilimia 73% ya malengo yaliyowekwa. Uzalishaji huo ulitokana na hekta 398,950 za mazao ya chakula na biashara zilizokuwa zimelimwa, ambazo ziliupatia Mkoa ziada ya mavuno ya jumla ya Tani 123,030 ya mazao ya chakula. Kati ya hizo tani 111,966 zilikuwa ni za wanga na tani 11,064 za mikunde.

**SEKTA YA USHIRIKA**

Kwa upande wa ushirika, kufikia siku ya kikao tayari minada kumi na mbili (12) ilikuwa imefanyika, ambapo Chama kikuu Lindi Mwambao kilikuwa kimefanya minada 6 na Chama kikuu cha RUNALI kilikuwa kimefanya minada 6. Aidha taarifa ilionesha kuwa, jumla ya kilo 45,604,538 zenye thamani ya TShs.106,924,033,478/= zilikuwa zimeshauzwa.

**SEKTA YA BIASHARA, VIWANDA NA UWEKEZAJI**

**Hali ya viwanda katika mkoa wa Lindi.**

Taarifa ilionesha kuwepo kwa ongezeko la viwanda 167 kutoka **437** vilivyokuwepo mwezi Januari, 2018 na kufikia jumla ya viwanda **604** mwaka 2020. Aidha, kati ya viwanda hivyo viwanda vidogo **597**, vya kati **5** na vikubwa **2**.

Taarifa ilionesha kuwa viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati ni vile vinavyojishughulisha na useremala, uchomeleaji, ufyatuaji tofali, ushonaji, ukamuaji mafuta ya alizeti, nazi na karanga, ubanguaji mdogo wa korosho na usindikaji wa unga wa muhogo

**Ugawaji wa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo (Wamachinga)mwaka 2020.**

Taarifa ilionesha kuwa mkoa ulipokea vitambulisho 30,000. Hadi kufikia tarehe 20 Novemba, 2020 vitambulisho 11,986 vyenye thamani ya Tsh. 239,720,000/= (sawa na

asilimia 33.29 %) vilikuwa vimegawanywa. Aidha, vitambulisho vilivyokuwa vimebaki ni 24,014 vyenye thamani ya Tsh. 480,280,000/= (sawa na asilimia 66.71%).

## SEKTA YA UVUVI

Taarifa ilionesha kuwa kuna takribani wavuvi 9,417 kukiwa na jumla ya vyombo vya uvuvi 2,437. Mpaka kufikia Julai, 2020 kulikuwa kuna jumla ya vikundi vya wavuvi wadogo wadogo 28 na Vyama 2 vya ushirika wa wavuvi ambavyo vimesajiliwa kisheria. Hadi kufikia Julai, 2020 jumla ya kilogramu 1,353,238.5 za samaki zilivuliwa zenye thamani ya Tsh. 5,481,269,500 kutokana na shughuli za uvuvi ndani ya mkoa.

Taarifa ilionesha kuwa suala la uvuvi haramu wa kutumia baruti lilikuwa limekwisha kwa asilimia 100 kutokana na jitihada za serikali kwa kushirikiana na jamii na wadau mbalimbali katika kupambana na uvuvi huo. Kufikia kipindi hicho mkoa ulikuwa umefanya doria 43 na kukamata makokoro 32, vyombo vya uvuvi 18, mideke 6 na aina nyingine za nyavu 37 ambazo haziruhusiwi kwa mujibu wa sheria ya uvuvi 2003 pamoja na kukamatwa kwa watuhumiwa 34 ambao walikutwa na makosa mbali mbali ya uvuvi na kuchukuliwa hatua. Katika kuimarisha usimamizi shirikishi wa raslimali za bahari mkoa umeunda vikundi vya ulinzi shirikishi vya rasilimali za bahari (BMU) 42.

## SEKTA YA MIFUGO

Taarifa liyowasilishwa ilionesha kuwa mkoa una jumla ya vijiji 51 vilivyotengwa kwa ajili ya wafugaji vyenye eneo la hekta zaidi ya 258,296.87 kwani kuna vijiji vingine bado havijapimwa. Kwa upande wa mauzo ya mifugo hai taarifa ilionesha kuwa, mkoa wa Lindi una jumla ya minada minane (8) ya mifugo ambapo minne inapatikana Kilwa, miwili manispaa ya Lindi, mmoja halmashauri ya wilaya Liwale na mmoja halmashauri ya wilaya ya Nachingwea. Minada inayofanya kazi ni minne na yote haijasajiliwa kutokana na ukosefu wa miundombinu inayohitajika.

## SEKTA YA MALIASILI

Taarifa iliyotolewa katika kikao ilionesha kuwa mkoa wa Lindi umepakana na mapori ya akiba (Hifadhi za Wanyama) **SELOUS** katika Wilaya za Liwale na Kilwa na **MSANJESI** katika Wilaya ya Nachingwea. Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Novemba, 2020 zaidi ya vijiji 80 vilitoa taarifa za kuonekana kwa wanyama wakali hususani tembo, nguruwe pori, nyati, fisi, simba na wengine.

Vijiji katika halmashauri za Mtama, Manispaa ya Lindi, Ruangwa, Liwale, Nachingwea, na Kilwa vililipoti kuvamiwa.

**SEKTA YA AFYA**

Katika kipindi hicho, sekta ilikuwa na majukumu yafuatayo:-

Kusimamia kujenga Vituo vya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na kujenga/kukarabati Hospitali, vituo vya Afya, Zahanati, mama ngonjea (Maternity waiting home) na nyumba za watumishi. Katika malengo hayo mkoa umefanikiwa kujenga hospitali mbili za wilaya ya Ruangwa, na Mtama, wodi ya wazazi katika hospitali ya Nachingwea. vituo 8 vya afya [Kibutuka; Liwale, Nkowe, na Mandawa-Ruangwa; Kitomanga- Lindi Manispaa; Kilimarondo-Nachingwea; Nyangamara- Mtama; Tingi na Kilwa Masoko- Kilwa] vimekamilika na kutoa huduma za upasuaji kwa uzazi pingamizi na mama wajawazito. Taaarifa ilieleza kuwa Hospitali ya Liwale ujenzi unaendelea na umefikia hatua ya umaliziaji kwa majengo mawili OPD na Maabara).

**SEKTA YA ELIMU**

Taarifa ya sekta ya elimu iliwasilishwa na kuonesha kuwa, kwa mwaka 2020/21 jumla ya Watahiniwa 19,632 walisajiliwa katika kufanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ambapo watahiniwa 19,388 walifanikiwa kufanya Mtihani ikiwa ni sawa na asilimia 98.76 na Watahiniwa 244 hawakufanya Mtihani huu. Taarifa iliyotolewa ilionesha kuwa Matokeo ya Mtihani yanaonesha kuwa, mwaka 2020, Mkoa umepata ufaulu wa 82.25% kutoka 76.48% mwaka 2019 ikiwa ni ongezeko la 6.77%. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania limeutaja Mkoa wa Lindi kuwa ni miongoni mwa Mikoa mitatu pekee iliyofanikiwa kupandisha ufaulu wake kwa miaka mitatu mfululizo.

**SEKTA YA MAJI**

Hadi kufikia mwezi Oktoba, 2020 asilimia 62.1 ya wakazi waishio vijijini katika mkoa wa Lindi, walikuwa wanapata huduma ya maji safi na salama kupitia miradi mbalimbali. Na asilimia 71 ya wakazi waishio mijini katika Halmashauri za Mkoa wanapata huduma ya maji safi na salama kupitia Mamlaka za Maji za maeneo husika.

**SEKTA YA UMEME**

Taarifa ilionyesha kuwa, katika mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya wateja wapya waliounganishwa na huduma ya umeme ni 7,608. Katika idadi hiyo wateja waliotokana na miradi ya umeme vijijini "REA" ni 2,611 na 4,997 wateja waliounganishwa na

TANESCO. Idadi hiyo ya wateja waliounganishwa na TANESCO ni sawa na asilimia 111% ya malengo. Jumla ya shule za msingi na sekondari na nyumba za walimu zilizounganishwa ni 81. Zahanati na nyumba za wauguzi zilizo unganishwa 34 na Vituo vya afya na nyumba za wauguzi 12.

**SEKTA YA ARDHI**

Taarifa ilionesha kuwa kazi zilizofanyika katika sekta ya ardhi ni pamoja na uandaaji wa hati na umilikishaji, usajili na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Aidha taarifa ilionesha kuwa jumla ya miliki za viwanja na mashamba (CROs) 751 zilikuwa zimetolewa, hatimiliki 268 zilikuwa zimesajiliwa, vyeti vya ardhi ya kijiji 3 vilikuwa vimetolewa. Katika kutekeleza maagizo mahsusi ya serikali, hatimiliki za kimila (CCROs) 622 zilikuwa zimetolewa katika ardhi ya vijiji katika halmashauri za wilaya za mkoa. Taarifa ilifafanua kuwa hadi wakati wa uandaaji taarifa migogoro ya matumizi ardhi 90 ilikuwa imetatuliwa.

**Baada ya mawasilisho hayo taarifa ilipokelewa na kujadiliwa kama ifuatavyo:-**

**Mkopo wa 2% kwa watu wenye walemavu**

Wakati wa mjadala wa taarifa ya mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ilijitokeza changamoto ya utekelezaji kwa upande wa vikundi vya watu wenye walemavu kutokana na kuwepo na ugumu wa kupata vikundi vya walemavu wanye mahitaji yanayofanana kwenye eneo moja ambavyo vitakidhi vigezo. Ulielezwa kuwa ushauri umepelekwa kwa Katibu Mkuu OR - TAMISEMI ili ikiwezekana mkopo utolewe kwa mnufaika mmoja mmoja. Aidha Idara ya Maendeleo ya jamii waendelee kutoa elimu kwenye maeneo yao ili makundi yote yajitokeze na kunufaika kama ilivyotarajiwa.

**Upungufu wa watumishi**:

Kwa upande wa changamoto za kiutendaji katika sekta zote hususan waalimu na waganga ilishauriwa kuwa taarifa inayoainisha mahitaji ya watumishi wa kada zote kimkoa iandaliwe ikionesha watumishi waliopo na upungufu kwa idadi na asilimia ili waheshimiwa wabunge wasaidie kujenga hoja katika mamlaka za ajira serikalini.

Mwenyekiti aliwakumbusha wajumbe kwamba utekelezaji wa mikopo ya asilimia 10 ya Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ni suala la kisheria na sio hiyari hivyo linapaswa kutekelezwa na fedha hizo hazitakiwi kukopwa kwa ajili ya kufanya shughuli nyingine.

**Ushirika**

Baadhi ya wajumbe walionesha wasiwasi wao juu ya kutochukua hatua kwa viongozi wa AMCOS na maafisa Ushirika kwa kuwa ili kuchukuliwa hatua ni mpaka kupata kibali kutoka kwa Mrajisi wa vyama vya Ushirika.

Ilielezwa kuwa maafisa ushirika hawana kinga ya mrajisi wanapofanya makosa ya jinai ila ni pale inapolazimika kuvunja bodi za vyama vya Ushirika ndio hapo mrajisi anapotakiwa kutoa kibali. Aidha, mkoa umejitahidi kufanya ufatiliaji kwenye maeneo yote yenye ubadhilifu na wahusika wanachukuliwa hatua. Hata hivyo changamoto kubwa ni baadhi ya viongozi ambao wameaminiwa na wakulima wenzao kupewa dhamana ya kuongoza badala yake wanakosa uaminifu. Hawa wanaendelea kushughulikiwa.

**Ubora wa zao la korosho:**

Wajumbe walishauri mkoa kupitia sekta husika uendelee kusimamia ubora katika ngazi zote kuanzia kwa mkulima, msafirishaji, maghalani na wauzaji wa jumla ili kutoharibu soko la ndani na nje ya nchi.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa ni kweli kwenye korosho kuna changamoto hiyo ya ubora hasa kwa korosho zinazotoka nje ya mkoa na mara zote kupitia Maafisa Kilimo kwenye halmashauri mkoa umeendelea kudhibiti korosho zote zisizo na ubora.

**Mifugo:**

Ilielezwa kuwa pamoja na eneo la mkoa kuwa kubwa kijiografia kulinganisha na idadi ya mifugo iliyopo ni vema changamoto ya mifugo kuingia kwenye maeneo ya wakulima na hifadhi za taifa likachukuliwa kwa uzito wake na tahadhari kubwa. Ushauri ulitolewa juu ya kuwepo na mkakati wa pamoja ili kudhibiti uingiaji holela wa mifugo ndani ya mkoa wetu ili lisiendelee kukua na kuleta madhara.

Katika kupitia taarifa ombi liliwasilishwa la kupata taarifa ya maendeleo ya kiwanda cha kuchakata gesi (LNG) eneo la Kikwetu. Ufafanuzi ulitolewa kuwa utekelezaji wa mradi wa LNG upo pale pale na Mhe. Rais amelisemea na kulipa uzito unaostahili baada ya kulipwa fidia mwezi Juni, 2020. Aidha suala hili lipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ukurasa wa 104 kipengere E suala la LNG ambako limeelezwa kwa kina.

**Wanyamapori:-**

Wajumbe walitoa pongezi kwa serikali kudhibiti ujangili na matokeo yake ni kuongezeka kwa wanyama ambao ni hatari kwa maisha ya binadamu, mazao na mifugo. Hivyo ushauri ulitolewa waombwe maaskari wa wanyamapori ili wawepo kila kata ili kudhibiti uharibifu kutokana na ukweli kuwa Mhe. Waziri Mkuu alishatoa agizo la kurejeshwa kwa kituo cha udhibiti wa wanyama maeneo ya Rondo na tayari Mkoa umeshawaandikia taasisi ya TAWA na ufuatiliaji unaendelea.

**Afya:-**

Lilitolewa angalizo kuwa pamoja na taarifa kuonesha kuwa katika udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI mkoa wetu unafanya vizuri bado tuchukue tahadhari wakati tukijipongeza kwani UKIMWI bado upo. Aidha kwa vile taarifa mbali mbali zinaonesha kuwa mkoa wa Lindi nimiongoni mwa mikoa mitano yenye maambukizi mengi ya malaria iwepo mikakati ya makusudi ya kutokomeza mbu na mazalia yake katika halmashauari zote.

**Elimu:-**

Katika majadiliano lilijitokeza suala la baadhi ya watu kutumia kambi za mada ngumu kama njia ya kupata wafuasi kipindi cha kampeni. Pia ilielezwa kuwa baadhi ya wazazi walishindwa kuwagharamia watoto wao na hivyo kukosa fursa ya kuhudhuria kambi za mada ngumu.

Mjumbe mmoja alishauri kuona uwezekano wa kila halmashauari kuwa na chuo cha VETA na ufafanuzi ukatolewa kuwa kwa sasa mkoa wetu bado una nafasi nyingi ambazo hazijajazwa katika chuo cha VETA Lindi na vyuo vya maendeleo ya wananchi (Folk Development Colleges) Kilwa na Chilala.

Ilielezwa kuwa chuo cha VETA – Lindi kina uwezo wa kuchukua wanafunzi 506 na miundombinu mizuri. Hata hivyo hadi sasa kimedahili wanafunzi 306 tu kutokana na idadi ndogo ya wanafunzi waliojitokeza. Hivyo viongozi waliombwa wahamasishe wananchi kupeleka watoto wao kwani ada ni Tsh. 120,000.00 kwa wanafunzi wa bweni na Tsh. 60,000.00 kwa wanafunzi wa kutwa.

**Nishati ya umeme:-**

Pamoja na wajumbe kupokea na kupongeza taarifa ya kazi zinazofanywa na shirika la umeme TANESCO, walionesha wasiwasi juu ya kuwepo na tatizo kubwa la kukatika kwa umeme mara kwa mara.

Wajumbe walitaka kujua sababu za hali hiyo na kama kuna changamoto yoyote ni vema ikawekwa wazi ili kuitafutia ufumbuzi wa kudumu kwani ukatikaji huo una athari kubwa katika suala zima la uwekezaji mkoani Lindi.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa hali ya umeme katika mkoa wa Lindi pamoja na juhudi za serikali za kuongeza vyanzo vya uzalishaji wa umeme kutoka kimoja cha Mtwara na kuongeza umeme wa Gridi kutoka Songea na Mbagala, njia za usambazaji na uchakavu wa mitambo ndiyo sababu ya kukatika kwa umeme mara kwa mara.

Aidha, meneja wa TANESCO kanda ya kusini alieleza kikao kuwa ili kuondokana na hali hiyo hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

a) Mwaka 2019 Serikali ilifunga mashine mpya 2 katika kituo cha uzalishaji cha Mtwara na hivyo kuwa na uwezo wa uzalishaji kufikia megawati 22 na wakati matumizi yalikuwa megawati 18 kwa mikoa ya Mtwara na Lindi.

b) Ili kupunguza mzigo mkubwa katika mitambo kwenye kituo cha Mtwara mkoa wa Lindi uliingizwa katika kupokea umeme wa Gridi ya taifa kutokea kituo cha Mbagala kwa umeme unaosambazwa maeneo ya Kilwa na baadhi ya maeneo ya Lindi vijijini. Aidha upo umeme mwingine wa Gridi ya taifa kutokea Songea ambao kwa kiasi kikubwa unasambazwa maeneo ya Masasi na Nachingwea.

c) Pamoja na juhudi hizo zilizofanyika changamoto kubwa inayoendelea kulikumba shirika la TANESCO ni laini za umeme kuwa ndefu sana na kukumbwa na vikwazo vya nguzo kuanguka na kusababisha kukatika kwa umeme

kusikotarajiwa. Aidha, lipo tatizo la watoto kutoka jamii zilizopo katika njia za usambazaji kupiga mawe vikombe katika nguzo na kusababisha hitilafu ya umeme kukatika, kwa hali hii shirika limelazimika kuingia gharama ya kubadili mfumo huo wa kutumia vikombe kwani ni hatari kwa mazingira ya sasa ndani ya jamii. Shirika la TANESCO liliomba wadau wote kufikisha elimu kwa wananchi kuhusiana na mazao yaliyopo chini ya miundombinu ya umeme hususan zao la Minazi ili wakubali kuondoa mazao hayo kwani nayo yanachangia kwa kiasi kikubwa kusababisha hitilafu.

d) Ili kumaliza tatizo hili TANESCO imeshaagiza mitambo mingine miwili mipya ambayo kila mmoja una uwezo wa kuzalisha Megawati 4 na hivyo uzalishaji wa umeme kwa kituo cha Mtwara utaongeeka kwa Megawati 8. Kazi ya kufunga mitambo imeshaanza na itakamilika mara baada ya mitambo kujaribiwa, kukidhi viwango na kupokelewa kwa mujibu wa taratibu za mikataba na manunuzi ya umma.

Lilijitokeza suala la wananchi wengi katika manispaa ya Lindi kufanya malipo ya kuunganishiwa umeme lakini wamechelewa kuunganishiwa kwa muda mrefu.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa ni kweli wananchi wengi walijitokeza na kuomba kufungiwa umeme baada ya serikali kupunguza gharama za kuunganisha umeme katika kipindi cha 2019/2020 na kufuatia hali hiyo shirika limeainisha mahitaji ya vifaa na kuhakikisha kuwa wote walioomba wanaunganishiwa umeme hadi kufikia Disemba, 2020.

Baada ya maelezo hayo mwenyekiti aliwaomba wajumbe ambao wanaingia Bungeni kusaidia mkoa kwa kuendelea kulisemea jambo hili la kukatika kwa umeme mara kwa mara ili wizara ikamilishe mipango na mkakati yake ya kuondoa changamoto hii.

**Elimu:-**

Katika suala la changamoto ya vituo vya mada ngumu ufafanuzi ulitolewa kuwa pamoja na baadhi ya wazazi kuonekana kutokuwa na uwezo wa kugharamia kambi hizi. Matokeo ya ufuatiliaji yanaonesha kuna mafanikio makubwa ya kuongeza kiwango cha ufaulu kimkoa. Pamoja na hayo ilifafanuliwa kuwa Suala la michango mashuleni, waraka wa elimu Namba 3 wa mwaka 2016 wa elimu bure haujakataza wazazi kuchangia maendeleo ya shule yao pale ambapo wamekubaliana.

Kikao kiliarifiwa juu ya kumalizika kwa mikataba ya waalimu waliokuwa wanajitolea kupitia mpango wa Mh. Waziri Mkuu ambao kwa kiwango kikubwa walisaidia kuongeza ufaulu kwenye mkoa wetu. Wajumbe walishauri ufuatiliaji ufanyike ili Serikali ifikirie kuongeza mkataba wao. Mkoa utaendelea kufuatilia baada ya kupeleka taarifa ya idadi ya watumishi kwenye sekta zote OR - TAMISEMI.

**Maagizo/Maazimio.**

i. **Katika kikao kijacho taarifa za kila halmashauri zioneshe orodha ya majina ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kiasi kilicho tengwa, kiasi kilicho tolewa kwa asilimia ya utekelezaji fedha zimetumika kiasi gani.**

ii. **TANESCO wahakikishe kuwa kazi ya ufungaji mitambo mipya katika kituo cha Mtwara inakamilika kwa wakati uliopangwa na kutoa taarifa ya hatua ya utekelezaji kwa Mkuu wa Mkoa ili awafikishie Wah. Wabunge na wadau wengine.**

iii. **Mameneja wa makampuni ya simu katika mkoa wa Lindi waalikwe na kushiriki katika kikao cha Bodi ya barabara siku ya tarehe 26/11/2020 ili kutoa ufafanuzi wa mipango ya kuongeza mawanda ya mawasiliano katika maeneo ya Mitwero.**

**Muht. Na. 08/11/2020: Taarifa ya hali halisi ya madawati, viti, meza na madarasa kwa shule za Sekondari na msingi hadi sasa**

Mwenyekiti aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kuwasilisha taarifa ya hali halisi ya madawati, viti, meza na madarasa kwa shule za sekondari na msingi katika kwenye halmashauri zao. Wakurugenzi walitoa taarifa kama ifuatavyo:-

**HALMASHAURI YA KILWA**

Halmashauri ya wilaya ya Kilwa ina jumla ya shule za msingi za serikali 108 zenye jumla ya wanafunzi 57,113 kati yao awali ni 5,136 na msingi ni 51,977. Mahitaji ya madawati ni 17,326 yaliyopo 14,695 sawa na asilimia 84.8 na upungufu ni 2,631 sawa na asilimia 15.2. Shule zenye upungufu mkubwa wa madawati ni 13 ambazo ni shule za msingi Njianne, Kibata, Mwengei, Mwangi , Mtende, Mandawa, Kiwawa, Kikotama, Mtoni, Kipindimbi, Somanga na Mzizima. Mahitaji ya vyumba vya madarasa ni 1,155 vilivyopo ni 746 sawa na asilimia 64.6 na upungufu ni 409 sawa na asilimia 35 . Kwa upande wa shule za sekondari Halmashauri ina jumla ya shule za sekondari 26 za Serikali ambazo kwa ujumla wake zina mahitaji ya viti 8,875 viti vilivyopo ni 8,594

upungufu ni 281 sawa na asilimia 3.2 na zina mahitaji ya meza 8,875 zilizopo ni 8,715 upungufu ni 160 sawa na asilimia 1.8. Mahitaji ya vyumba vya madarasa ni 85 vilivyopo ni 50 sawa na asilimia 58.8 na upungufu ni 35 sawa na asilimia 41. upungufu huo uko katika baadhi ya shule na tayari mikakati ya kuondoa upungufu huo imewekwa na halmashauari kama ifuatavyo:-

i. Mwaka 2020/2021 Halmashauri imetenga jumla ya Tsh. 56,000,000.00 kwa ajili ya madawati, viti na meza kati ya hizo Tsh. 10,920,000 ni kwa ajili ya kutengeneza seti 156 za viti na meza katika shule za sekondari na Tsh. 45,080,000 kwa ajili ya kutengeneza madawati 644 ya shule za msingi Wataendelea kutenga kila mwaka.

ii. Ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa viendane na utengenezaji wa viti na meza katika kila darasa linalojengwa.

iii. Mwaka 2020/2021 Halmashauri imetenga kiasi cha Tshs.555,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji na ujenzi wa vyumba 39 vya madarasa kwa shule za msingi na sekondari, ambapo madarasa 19 ni shule za sekondari kwa gharama ya Tshs. 320,000,000.00 na 20 kwa shule za msingingi kwa gharama ya Tshs. 235,000,000.00

iv. Kusimamia na kufuatilia matumizi ya fedha za fidia ya ada na capitation kukarabati madawati, viti na meza shuleni ambapo kwa mwaka 2019/2020 jumla ya viti 102 na meza 73 zilikarabatiwa.

v. Kuhamasisha serikali za vijiji, jamii, vyama vya ushirika na wadau wa maendeleo kujenga madarasa na kutengeneza viti, meza na madawati na kuvikabidhi shuleni ili kupunguza tatizo la upungufu wa samani.

## HALMASHAUARI YA WILAYA YA LIWALE

Halmashauri ya Wilaya ya Liwale katika sekta ya elimu msingi ilikuwa na upungufu ya meza za walimu 430, upungufu wa Viti vya walimu 414, upungufu wa Madawati 106. Upungufu huu umesababishwa na uchakavu na uharibikaji wa samani hizo. Pia kuna upungufu wa madarasa 169. Jitahada za umaliziaji wa ujenzi wa madarasa mashuleni unafanyika. Aidha, halmashauri ina mahitaji ya madawati 8347 kwa shule za msingi na yaliyopo ni 8241 na kuwa na upungufu wa madawati 106. Kwa upande wa madarasa mahitaji ni 570, yaliyopo ni 401 na upungufu ni 169.

Katika sekta ya elimu sekondari kuna mahitaji ya meza za wanafunzi 4133 na zilizopo ni 4524 ziada ikiwa ni meza 391. Aidha, mahitaji ya viti ni 4133 na vilivyopo ni viti 4459 hivyo kuna ziada ya viti 321, Kwa upande wa madarasa mahitaji ni 125 yaliyopo ni 133 na kuna ziada ya madarasa 8.

**Maandalizi ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza 2021**

Taarifa ilifafanua kuwa,halmashauri ya Liwale inaendelea kufanya jitihada ya kuhakikisha wanafunzi wote wanaofaulu elimu ya msingi wanasajiliwa kuingia kwenye kidato cha kwanza kwa kuandaa madarasa, viti na meza kwa kuzingatia maoteo ya wanafunzi ya mwaka 2021.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA**

Taarifa iliyotolewa ilionesha kuwa Halmashauri ya Nachingwea ina jumla ya shule za msingi 108 (shule za serikali 105 na binafsi 3) zinazotoa Elimu ya awali na Msingi. Kwa mwaka wa fedha na 2019/2020 tulipokea fedha jumla ya Tsh. 1,103,693,000 za EP4R na mapato ya ndani Tsh. 41,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 71 kwa shule 40 na Tsh. 175,778,504.77 za program ya SWASH na mapato ya ndani ya Tsh. 18,000,000 kwa ajili ya ujenzi mpya wa matundu ya vyoo 140 kwa shule 7. Aidha hali ya madawati kwa shule zote za msingi kulingana na idadi ya wanafunzi 43379 inaonesha kuwa mahtaji ni madawati 14460 yaliyopo ni 13167 na hivyo kuwa na upungufu wa madawati 1293.

Mikakati iliyowekwa na halmashauari ni kutumia mapato ya ndani ambapo halmashauri imetoa jumla ya Tsh. 41,489,000.00 kwa ajili ya utengenezaji wa madawati 1,095 ambapo madawati 993 yameshakamilika na yaliyosalia 102 yanaendelea kutengenezwa kwa awamu ya kwanza na kwa awamu ya pili madawati 1191 yanatarajiwa kutengenezwa kuanzia mwezi januari, 2021 ili kumaliza na changamoto ya madawati iliyopo.

Halmashauri ya Nachinwea bado ina upungufu wa miundombinu ya vyumba vya madarasa kwa shule zenye idadi kubwa ya wanafunzi lakini pia kwa shule mpya zinazoanzishwa kwenye maeneo yenye shule shikizi ambazo tayari jamii imeanza kujenga baada ya kuhamasishwa na kushirikiana na Halmashauri. Kwa maoteo ya 2021 kutakuwa na wanafunzi 43379 na mahitaji ya madarasa ni 1342 yaliyopo ni 689 na hivyo kuwa na upungufu wa madarasa 653.

Kupitia fedha za ndani, wafadhili na serikali kuu, halmashauri imeweka mpango wa kujenga na kukamilisha madarasa yaliyoanzishwa na jamii katika shule zinazoendelea, shule shikizi na shule mpya ili kuondoa tatizo la upungufu wa madarasa kwa muda wa miaka mitano ijayo. Aidha, imeweka mpango wa kumalizia miradi ya madarsa 35 ya shule 23 za msingi katika mwaka wa fedha 2020/2021 kupitia fedha za mapato ya ndani shilingi 112,500,000.00 na madarasa 26 kupitia fedha za ruzuku ya serikali kuu na wafadhili shilingi 325,000,000.00.

**Mahitaji ya Vyumba vya madarasa vya kidato cha kwanza 2021**

Kwa ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba, mwaka 2020 wanafunzi 2173 watahitaji vyumba vya madarasa 44 na yaliyopo ni 21 na kuwa na upungufu wa vyumba 23 na kwa changamoto hiyo ya upungufu wa vyumba vya madarasa baadhi ya shule zitatakiwa kujenga vyumba vipya vya madarasa.

**Mpango wa ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya kidato cha I-2021:**

i. Kuomba fedha zilizotengwa kwa ajili ya umaliziaji na ujenzi wa madarasa kwenye mwaka wa fedha 2020/2021 kutoka OR-TAMISEMI

ii. Kuwahamasisha wananchi na wadau wengine kuchangia ujenzi wa madarasa katika maeneo yenye uhaba

Pamoja na mipango hiyo halmashauri ina mpango mkuu wa muda mrefu wa kutatua tatizo la madarsa na madawati kupitia mpango wake wa kujenga shule moja kubwa ya bweni ya wavulana ambayo itakuwa mkombozi.

**Mikakati ya kupunguza changamoto ya samani za wanafunzi**

i. Kutengeneza samani kupitia mapato ya ndani

ii. Kuwaomba Wadau kuchangia kwenye utengenezaji wa samani za wanafunzi.Halimashauri imepata mdau wa Elimu ambaye atatengeneza meza 1,400 na viti 1,400.

iii. Kukarabati samani za wanafunzi kupitia fedha za Elimu bila malipo

## HALMASHAURI YA MTAMA

### Hali halisi ya samani katika shule za msingi

Tarifa ilionesha kuwa halmashuri ina mahitaji ya madawati 10691 na yaliyopo ni 10327 na hivyo kuwa na upungufu wa madawati 364. Aidha, mahitaji ya vyumba vya madarasa ni 823, yaliyopo ni 490 na kuwa na upungufu wa madarasa 333.

### Hali halisi ya samani katika shule za sekondari

Halmashauri imefanikiwa kutengeneza meza na viti ili kupunguza uhaba wa samahi hizo uliopo katika shule za sekondari na hadi sasa mahitaji ni meza 5883 zilizopo ni 4423 na hivyo kuwa na upungufu wa meza 1460. Aidha kuna mahitaji ya viti 5883 na vilivyopo ni 4530, upungufu ukiwa ni viti 1353. Vyumba vya madarasa vinahitajika 53 na vilivyopo ni 44 na kuwa na upungufu wa vyumba 9.

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

Halmashauri ya manispaa ya Lindi ilikuwa na uhitaji wa jumla ya meza 7,184 na viti 7,184 kwa ajili ya wanafunzi wa shule za sekondari 17. Hata hivyo, Meza zilizopo ni 6,400 na Viti 6,339 na kufanya upungufu wa meza 1,019 na viti 1,084. Aidha, halmashauri ya Manispaa ya Lindi ina uhitaji wa jumla ya madawati 9,999 kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi. Hata hivyo, Madawati yaliyopo ni 8498 na upungufu wa madawati 1501.

**Mkakati wa kukabiliana na Upungufu wa Madawati, Viti na Meza za wanafunzi.**

Katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa madawati, viti, meza na samani zingine za ofisini, halmashauri ya manispaa ya Lindi ilipitisha azimio la kununua Mashine na vifaa vyote vinavyohitajika kwa ajili ya kuanzisha karakana ya useremala ili kuwezesha matengenezo ya samani mpya na ukarabati wa samani zilizoharibika kwa kutumia wataalamu waliopo. Aidha, Mbao kwa ajili ya kutengeneza samani hizi tunatarajia kutoka katika misitu iliyopo katika Vijiji vyetu na zingine zitapatikana kupitia kwa wakala wa misitu(TFS). Mashine na vifaa kwa ajili ya karakana vimeshanunuliwa na hadi kufikia tarehe 01 Desemba, 2020 vitakuwa vimeshafungwa tayari kuanza uzalishaji wa samani za mashuleni ili ifikapo tarehe 30 Januari 2021 pasiwepo tena upungufu wa madawati, viti na meza katika shule zote.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

Taarifa ilonesha kuwa, Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa ina jumla ya shule za msingi 82 ambazo zinahitaji jumla ya madawati 12,118 yaliyopo ni 11,939 na pungufu ni 179, meza mahitaji ni 1,081, zilizopo ni 645 na pungufu ni 436, viti mahitaji ni 1206, vilivyopo ni 667 na pungufu ni 569.

Kwa upande wa vyumba vya madarasa mahitaji ni 815, vilivyopo ni 534 na pungufu ni 281, nyumba za walimu mahitaji ni 595, zilizopo ni 210 na pungufu ni 385, vyoo vya wanafunzi mahitaji ni 584, vilivyopo ni 398 na upungufu ni 186 na vyoo vya walimu mahitaji ni 182, vilivyopo ni 113 na pungufu ni 69.

Kwa sasa halmashauri inaendelea na mikakati mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu kwa kujenga madarasa mapya 36 pamoja na samani zake (kwa maana ya viti na meza), vyoo vipya 338 na nyumba 1 ya walimu (2 in 1) ili kuweza kupunguza uhaba wa miundombinu katika shule za msingi.

**Hali halisi kwa shule za sekondari**

Kwa upande wa Sekondari, halmashauri ina jumla ya shule za sekondari 21. Shule hizi zinahitaji jumla ya meza 5,254, zilizopo ni 5,608 na kuwa na ziada ya 354, pia viti mahitaji ni 5,254, vilivyopo ni 5,319 na kuwa na ziada ya 65. Halmashauri itafanya msawazo kutoka shule zenye ziada kwenda shule zenye mapungufu.

Kwa sasa halmashauri inaendelea na mikakati mbalimbali katika kukabiliana na changamoto za upungufu wa miundombinu kwa kujenga madarasa mapya 23 pamoja na samani zake (viti na meza), maabara 6 na samani zake, nyumba za walimu 2, mabweni 6 na samani zake na vyoo vipya 12, juhudi hizi zinalenga kupunguza ama kumaliza kabisa tatizo la uhaba wa miundombinu kwa shule za sekondari.

**Maandalizi ya kuwapokea wanafunzi kidato cha kwanza mwaka 2021.**

Kwa mwaka 2021 halmashauri ya wilaya Ruangwa itakuwa na jumla ya wanafunzi 2,291 (wav 1075, was 1216) waliofaulu mtihani wa darasa la saba tayari kwa kujiunga na kidato cha kwanza, ambao watahitaji jumla ya madarasa 65 ikiwa yaliyopo ni 61 hivyo kuwa na upungufu wa madarasa 4.

Kwa upande wa samani, vinahitajika viti 2,371 ikiwa viti vilivyopo ni 1,524 na upungufu wa viti ni 847 na meza zinazohitajika ni 2,371 zilizopo ni 1,468 na upungufu wa meza ni 903

**Mkakati ya kukabiliana na upungufu:-**

i. Kujenga vyumba 2 vya madarasa katika shule ya sekondari Mnacho, ujenzi umefikia hatua ya linta na ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 katika shule ya msingi Likunja ambapo ujenzi umefikia hatua ya kuezeka kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.

ii. Kuendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa 14, matundu ya vyoo 12, mabweni 6 na mabwalo 2 kwa fedha za kutoka serikali kuu EP4R.

**Maagizo/maelekezo mahususi:-**

i) Kila mkurugenzi ahakikishe kuwa ifikapo mwezi Januari, 2021 wakati shule zinafunguliwa isitokee kiongozi yeyote kutoa taarifa ya upungufu wa samani shuleni kwani muda wa kujipanga bado upo.

ii) Mkuu wa Mkoa akishirikiana na wataalamu wa Sekretarieti ya Mkoa atapita kwa njia ya ziara ya kushtukiza kukagua kabla ya kufika kipindi hicho kwani kila halmashauri inajua idadi ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba kila mwaka na hakuna sababu ya kusubiri.

iii) Mkuu wa Mkoa akikuta shule yoyote haina vyoo ataifunga shule hiyo na viongozi wa Halmashauri husika watajieleza kuhusiana na hali hiyo.

iv) Kuanzia sasa mkoa hautaruhusu ujenzi wa madarasa bila ya ujenzi wa ofisi za walimu kwenye miradi yote ya ujenzi wa madarasa utakaofanyika hivyo hakuna shule itakayofunguliwa bila kuwa na ofisi za walimu.

v) Madarasa yaliyochakaa yakarabatiwe kupitia fedha za "capitation".

Agizo/Azimio

i. **Kuna maeneo ambayo fedha "capitation"zinatumika vibaya, hivyo hadi kufikia Machi, 2021 halmashauri zifanye ukaguzi na kutoa taarifa ya matumizi ya fedha hizo kwa RAS ili aifikishe kwa Mkuu wa Mkoa.**

**Muht. Na. 09/02/2020: MENGINEYO**

**a) KODI KATIKA SHUGHULI ZA KILIMO**

Mwenyekiti alimwalika meneja wa TRA mkoa wa Lindi kutoa kwa muhtasari juu ya nia ya kuanza kutoza kodi katika shughuli za kilimo. Mwasilishaji alianza kuelezea maana ya kodi kuwa ni malipo ya lazima ambayo serikali inawatoza wananchi wake ili kuendesha shughuli zake kwa manufaa ya wananchi wake na ni chanzo kikuu cha mapato kwa serikali yoyote ile. Mapato haya yanagharamia shughuli mbalimbali za serikali hususani mishahara na huduma za kijamii kama Shule, Hospitali, ulinzi nk

Ufafanuzi ulitolewa kuwa kuna aina kuu mbili za kodi nchini ambazo ni **kodi ya moja kwa moja (Direct tax) ambayo** ni kodi inayotozwa kwa mtu yeyote anaye pata pato litokanalo na vyanzo vikuu vitatu ambavyo ni ajira, uwekezaji na biashara. Aidha, aina ya pili ni **kodi isiyo ya moja kwa moja (Indirect taxes**) ambayo inalipwa kutokana na jinsi mtu anavyotumia bidhaa au huduma ambayo inaitwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) nk kodi hii mara zote inalipwa na mtu mwingine na kuwasilishwa TRA na mtu mwingine.

**Kilimo na kodi**

Ilielezwa kuwa mapato yatokanayo na shughuli za kilimo yanatozwa kodi na haya ni mapato ya wakulima wadogowadogo ambao wanatumia mavuno kujikimu kimaisha, Mauzo ghafi yao hayazidi Tsh. 4,000,000 kwa mwaka na hawa ni wale ambao hawana shughuli nyingine yoyote (yaani hawana kipato kingine zaidi ya kilimo). Pia kuna mapato yatokanayo na kilimo kinachojiendesha kibiashara na hawa ni wale ambao mauzo ghafi yao ni zaidi ya Tsh. 4,000,000 kwa mwaka.

**Wajibu wa kuwasilisha marejesho ya kodi (Tax Return)katika shughuli za kilimo.**

Ilielezwa kuwa kwa mkulima ambaye mauzo yake ghafi yapo kati ya Tsh. 4,000,000 na 100,000,000 kwa mwaka hapaswi kuwasilisha ritani na hesabu za mapato. Aidha kwa mkulima anayeuza mazao ya kilimo na mauzo hayo ni zaidi ya Tsh. 100,000,000 kwa mwaka, kama wafanyabiashara wengine wanapaswa kulipa kodi yake kutokana na faida anayopata na hivyo anawajibika kuwasilisha ritani ya hesabu zake.

**Jinsi Mfanyabiashara ya Kilimo anavyo lipa kodi na kuwasilisha ritani yake.**

Ilielezwa kuwa kwa mkulima anayejishughulisha na mazao ya msimu, makadirio ya kodi yatalipwa kwa awamu mbili kwanza ni mwezi wa tisa na mwezi wa kumi na mbili kwa kila mwaka. Aidha, kwa wafanyabiashara ya kilimo ambao mauzo yao hayazidi Tsh. 100,000,000 watalipa kodi kwa kadiri ya mauzo au faida na kama wataamua kukadiriwa kwa kadiri ya mauzo, basi kodi itakadiriwa kulingana na viwango kama inavyoeleza hapa chini

**Uwasilishaji wa Ritani**

Ilielezwa kuwa kwa upande wa Mkulima Mdogo ambaye mauzo ghafi ya mazao yake yatokanayo na kilimo yanazidi Tsh. 4,000,000/= na hayazidi Tsh.100,000,000/= kwa mwaka hapaswi kuwasilisha Ritani wala kutengeneza hesabu za Mapato na matumizi. Na kwa upande mwingine, yule ambaye mauzo yake ya kilimo yanazidi kiwango cha Tsh. 100,000,000 kwa mwaka anawajibu wa kuwasilisha ritani na hesabu ya mapato na matumizi.

**Kodi ya bidhaa na ushuru wa forodha kwenye mazao ya kilimo**

Hakuna kodi katika uuzaji mazao ya kilimo nje ya nchi, isipokuwa:-

- ✓ 15% ya thamani ya korosho zisizobanguliwa au Dola 160 kwa Tani,
- ✓ 80% ya thamani ya ngozi ghafi au Dola 0.52 kwa kilo hizi zote hutegemea kiwango kipi ni kikubwa bidhaa zinazosafirishwa nje ya Nchi hutozwa kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha Sifuri.

**Kusajiliwa** VAT

- ✓ Kwa Mfanyabiashara anayejihusisha na vifaa vya kilimo pekee hastahili kusajiliwa VAT hata kama mauzo yake kwa mwaka ni zaidi ya Tsh. 100,000,000/=
- ✓ Endapo mfanyabiashara anashughulika pia na kuuza bidhaa zinazotozwa kodi ya ongezeko la thamani na mauzo yake kwa mwaka yanazidi Tsh. 100,000,000/= atasajiliwa katika VAT.
- ✓ Marejesho ya kodi ni kwa uwiano wa 90% kwa bidhaa zinazotozwa kodi dhidi ya bidhaa zisizotozwa kodi.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa na wajumbe na walio wengi walihofia kuleta mkanganyiko kati ya tozo zilizofutwa na serikali na utozaji wa kodi hii. Aidha, kwa vile kodi hii inahusu nchi nzima TRA mkoa wameshauriwa wasianze utekelezaji katika mkoa pekee bali utekelezaji uwe kwa nchi nzima.

**Muht. Na. 09/02/2020: Kufunga Kikao**

Kabla ya kufunga kikao mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na aliendelea kuwakumbusha wajumbe na watumishi wengine kuzingatia nidhamu za vikao kwa kukaa hadi mwisho wa vikao.

Aidha, alitoa taarifa kuwa mkoa wetu upo kwenye eneo la mpakani ambapo baadhi ya raia wa Tanzania wanashirikiana na raia wa Msumbiji ambao wanaihujumu Serikali ya Msumbiji. Yapo matukio ya kihalifu ambayo yameanza kujitokeza. Kwa hali hii alitoa wito kwa wadau wote kuwakumbusha wananchi kuchukua tahadhari hasa wanapopokea wageni ambao hawawafahamu. Alitoa angalizo kuwa wageni hao wanakuja na sura tofauti ikiwemo uwekezaji, kilimo, biashara, wahubiri wa dini, uchimbaji madini, ufugaji, uvuvi n.k. Aidha, vipo viashiria kuwa kuna mahusiano kati ya wananchi wa Tanzania na wahalifu wa Msumbiji na wakati mwingine raia wa Tanzania wameonekana kuvuka na kwenda upande wa pili wa mpaka nchini Msumbiji bila kufuata taratibu za uhamiaji.

Aliwataka viongozi wote katika ngazi ya wilaya na halmashauri kusimamia kikamilifu minada ya korosho inayoendelea na kuhakikisha kuwa wakulima hawadhulumiwi. Alisisitiza na kuwataka viongozi wa TANESCO mkoa wa Lindi kushirikiana na ofisi ya Kanda iliyoko Mtwara kuweka bidii zaidi katika kutatua changamoto za kukatika kwa umeme mara kwa mara kwenye mkoa wa Lindi.

Katika kuimarisha uwajibikaji aliwakumbusha wakuu wote wa taasisi za umma na wakuu wote wa idara za serikali wahakikishe wanakuwa na nakala ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020 ili kufuatilia na kutekeleza maagizo pasipo kusubiri kusukumwa.

Mwisho alitoa taarifa kuwa kikao kijacho kifanyike mwezi Februari, 2021 na wahusika wote wawe wametekeleza maazimio na makubaliano ya kikao bila kusubiri kutumiwa muhtasari kwani kila mmoja alikuwa akifuatilia na kununukuu maeneo yanayomuhusu. Kikao kilifungwa rasmi saa 10.58 Jioni.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

Mwenyekiti

Katibu

Tarehe 16/3/2022

# Yatokanayo na Muhtasari wa Kikao cha tarehe 25.11.2020

YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA KWANZA CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA KILICHOFANYIKA UKUMBI WA OFISI YA MKUU WA MKOA TAREHE 25.11.2020.

| Muhtasari Na. | Azimio/Maagizo | Mtekelezaji | Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| **Muht. Na. 04/11/2020:Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya kikao cha tarehe 28 Februari, 2020** | i. Mkurugenzi wa halmashauri ya Mtama ahakikishe kuwa Tsh. Milioni 200 zilizotengwa katika bajeti zinaelekezwa katika ujenzi wa kituo cha mabasi na kazi iwe imekamilika katika kipindi cha miezi mitatu toka tarehe ya kikao. | Mkurugenzi Mtendaji - Mtama | Utekelezaji umefanyika kwa kufanya matengenezo madogo madogo kama kujaza kifusi na kujenga kibanda kimoja cha mlinzi kwa gharama ya Shs. 5,400,000.00 |
| | ii. Katika kipindi cha miezi mitatu Wakurugenzi wa halmashauri za Kilwa na Nachingwea wakamilishe ujenzi wa vituo vya mabasi vya Nangurukuru – Kilwa na Nachingwea. | Wakurugenzi watendaji Kilwa na Nachingwea | **Kilwa –DC**<br>**Agizo limezingatiwa,** Ujenzi wa kituo cha mabasi awamu ya kwanza katika eneo la Nangurukuru upo katika hatua ifutayo:- Kamilisheni<br><br>Kazi ya vyoo imekamilika na kazi inayoendelea ni kujenga mabanda ya kupumzikia abiria ili wasiathirike na mvua na jua. Aidha Halmashauri inafuatilia maombi yaliyowasilishwa TAMISEMI/HAZINA kupitia kitengo cha miradi ya kimkakati kwa ajili uendelezaji wa stendi ya kisasa.<br><br>**Nachingwe – DC**<br>Ujenzi wa kituo cha mabasi (Stendi Mpya) umekamilika na stendi inatumika. |
| | iii. Halmashauari ya Wilaya ya Kilwa iweke katika mipango yake ujenzi wa kituo cha Afya Kipatimu. | Mkurugenzi Mtendaji Kilwa | **Agizo limezingatiwa**, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri imeanza ujenzi wa kituo cha Afya katika Kata ya Chumo ambacho kinakusudiwa kutoa huduma kwa wananchi wa Kata za Kipatimu, Kibata, Chumo na kata ya Namayuni. Kwa kuwa kuna mahitaji ya kuwa na kituo cha Afya katika kata ya Kipatimu na kwa kuwa sera ya chama cha Mapinduzi ni kuwa na |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | kituo cha Afya kila Kata Halmashauri itaweka katika mipango yake ujenzi wa kituo cha Afya kata ya Kipatimu. |
| | iv. | Katibu Tawala Msaidizi Utawala na Raslimali Watu RS Lindi aandae kikao kati ya Katibu Tawala wa Mkoa na Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki – Lindi kujadili kwa pamoja malalamiko ya wananchi wa Kipatimu juu ya huduma inayotolewa katika Kituo cha Afya Kipatimu. | Katibu Tawala Msaidizi Utawala na Raslimali Watu | Mawasiliano yalifanyika na timu ya mkoa iliongea na baba Askofu na pia iliweza kufika Kituo cha Afya Kipatimu kusikiliza malalamiko ya wananchi na pande zote zilifikia muafaka. |
| **Muht. Na. 05/11/2020: Taarifa ya uchaguzi Mkuu Oktoba, 2020** | i. | Kamanda wa polisi wa mkoa afuatilie mienendo ya majalada yote ya uchunguzi na kuhakikishga kuwa wote waliohusika wanakamatwa, uchunguzi kukamilika na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria ili haki itendeke. | RPC | Ufuatiliaji ulifanyika na watuhumiwa wote waliohusika walifikishwa mbele ya vyombo vya sheria. |
| | ii. | Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Lindi kupitia Kamati ya Usalama ya wilaya ya Lindi ihakikishe kuwa anafuatilia suala la mtuhumiwa aliyekamatwa na kuachiwa na ikishindikana suala hilo lipelekwe kwenye kamati ya usalama ya mkoa. | DC Lindi | Mtuhumiwa alifuatiliwa na hatua za kisheria zilifuatwa. |
| ***Muht. Na. 07/11/2020: Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kuanzia Julai, 2020/2021 hadi Oktoba, 2020*** | i. | Halmashauri zioneshe orodha ya majina ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na kiasi kilichotengwa, kilichotolewa kwa asilimia ya utekelezaji fedha zimetumika kiasi gani. | Wakurugenzi wa halmashauri. | Agizo limetekelezwa, orodha imeambatishwa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | ii. TANESCO wahakikishe kuwa kazi ya ufungaji mitambo mipya katika kituo cha Mtwara inakamilika kwa wakati uliopangwa na kutoa taarifa ya hatua ya utekelezaji kwa Mkuu wa Mkoa ili awafikishie Wah. Wabunge na wadau wengine. | Meneja TANESCO Mkoa wa Lindi | Kazi ya ufungaji mitambo mipya imekamilika tangu mwezi wa kumi na mbili 2020. Mitambo hii bado ipo chini ya uangalizi wa mkandarasi kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa mujibu wa mkataba wake. Aidha, ataendelea kurekebisha hitilafu zozote zitakazokuwa zinajitokeza. |
| | iii. Mameneja wa makampuni ya simu katika mkoa wa Lindi waalikwe na kushiriki katika kikao cha Bodi ya barabara siku ya tarehe 26/11/2020 ili kutoa ufafanuzi wa mipango ya kuongeza uwanda/wigo wa mawasiliano katika maeneo ya Mitwero. | RAS | Mameneja wote wa makampuni ya simu katika mkoa wa Lindi walialikwa na kuhudhuria kikao cha Bodi ya barabara siku ya tarehe 26/11/2020 kama ilivyoagizwa. |
| **Muht. Na. 08/11/2020: Taarifa ya hali halisi ya madawati, viti, meza na madarasa kwa shule za Sekondari na msingi hadi sasa** | i. Kuna maeneo ambayo fedha "capitation" zinatumika vibaya, hivyo hadi kufikia Machi, 2021 halmashauri zifanye ukaguzi na kutoa taarifa za matumizi ya fedha hizo kwa RAS ili afikishe kwa Mkuu wa Mkoa. | Wakurugenzi wa halmashauri. | Agizo lilitekelezwa na taarifa iliwasilishwa. |